Baraka Ya Kikuhani

na

Ellis Forsman

Baraka Ya Kikuhani

na

Ellis Forsman

Oktoba 15, 2011

Baraka Ya Kikuhani

Hesabu 6:22-27

Katika kitabu ambacho kimejawa na "hesabu", tunakuta kwamba mfungamano wa maandiko, ambayo imeitwa "Sala ya Bwana ya Agano la Kale":

Hes. 6:22-27, "*Kisha BWANA akanena na Musa, na kumwambia, nena na Haruni na wanawe, uwaambie hivi ndivyo mtakavyowabarikia wana wa Israeli, mtawaambia; BWANA akubarikie na kukulinda; BWANA akuangazie nuru za uso wake, na kukufadhili; BWANA akuinulie uso wake, na kukupa amani. Ndivyo mtakavyoweka jina langu juu ya wana wa Israeli; nami nitawabarikia.*"

Kama ilivyoangaliwa katika andiko hili, ni Baraka za Bwana ndiyo Aruni na wanawe wangewabarikia wana wa Israeli. Aruni na wanawe walifanya ukuhani kwa Israeli.

Hivyo mara zote kifungu hiki kimekuwa kikiitwa "Baraka ya Kikuhani" (pia mfungano wa Kiaruni).

Katika kifungu hiki tunajifunza vitu kumhusu Bwana ambazo ni kweli leo.

Hata ivyo hatuishi chini ya Agano ya Kale, pamoja na ukuhani wake wa Kiaruni, bali tuna "Kuhani Mkuu", ambaye hutamani kutubariki zaidi (kama si zaidi).

Ili kuelewa ninacho maanisha, hebu tuangalie kwa karibu zaidi juu ya …

Fafanuzi ya Baraka ya kikuhani

"*Bwana akubariki na kukulinda.*" (Hes. 6:24).

Neno "*bariki*" inamanisha "kuwa salam au mafanikio".

Ahadi ya Baraka kama hizo ilikuwa ni lazima.

Kumb. 28:1-6, "*Itakuwa utakaposikia sauti ya BWANA Mungu wako, kwa bidii kutunza kuyafanya maagizo yake nikuagizayo leo, ndipo BWANA Mungu wako atakapokutukuza juu ya mataifa yote ya dunia; na Baraka hizi zote zitakujilia na kukupata usikiapo sauti ya BWANA Mungu wako. Utabarikiwa mjini utabarikiwa na mashambani. Utabarikiwa uzao wa tumbo lako, na uzao wan chi yako, na uzao wa wanyama wako na mifugo, maongeo ya ng'ombe wako na wadogo wa kondoo zako, litabarikiwa kapu lako na chombo chako cha kukandia unga. Utabarikiwa uingiapo, utabarikiwa na utokapo.*"

Kushindwa kutimiza maagizo ya Bwana huleta laana, siyo Baraka.

Kumb. 28:15-19, "*Lakini itakuwa usipotaka kuisikiza sauti ya BWANA Mungu wako, usiyaangalie kufanya maagizo yake yote na amri zake, nikuagizayo hivi leo, ndipo zitakapokujia laana hizi zote na kukupata. Utalaaniwa mjini utalaaniwa na mashambani. Litalaaniwa kapu lako na chombo chako cha kukandia. Utalaaniwa uzao wa tumbo lako, na uzao wan chi yako, maongeo wa ng'ombe wako, na wadogo wa kondoo zako. Utalaaniwa uingiapo utalaaniwa na utokapo.*"

Neno "tunza" inamanisha kutoa huduma na kujali, kulinda na kukinga.

Zaburi nzuri inayoongelea Mungu anavyojali ni:

Zab. 121:1-8, "*Nitayainua macho yangu niitazame milima, msaada wangu utatoka wapi? Msaada wangu u katika BWANA, aliyezifanya mbingu na nchi. Asiuache mguu wako usogezwe; asisinzie akulindaye; naam hatasinzia wala hata lala usingizi, yeye aliyemlinzi wa Israeli. BWANA ndiye mlinzi wako; BWANA ni uvuli mkono wako wa kuume. Jua halitakupiga mchana, wala mwezi wakati wa usiku. BWANA atakulinda na mabaya yote, atakulinda nafsi yako. BWANA atakulinda utokapo na uingiapo, tangu sasa na hata milele.*"

Ni kama mchungaji anapolinda na kuwaongoza kondoo, wito uliyofungana juu ya Mungu kutunza na kuangalia Israeli.

"*BWANA akuangazie nuru ya uso wake na kukufadhili;*" (Hes. 6:25).

Kufanya "*uso wake ung'ae*" labda ni dhahiri, ikionyesha tabasamu ya Mungu dhidi ya watu wake, ikithibitisha kuwa kwake mwenye rehema.

Angalia jinsi inavyotumiwa sehemu nyingine:

- Zab. 31:16, "*Umwangaze mtumishi wako kwa nuru ya uso wako; uniokoe kwa ajili ya fadhili zako.*"
- Zab. 80:3, "*Ee Mungu uturudishe, uangazishe uso wako nasi tutaokoka.*"
- Dan. 9:17, "*Ee Bwana usikie; Ee Bwana usamehe, Ee Bwana usikilize ukatende usikawie; kwa ajili yako wewe, Ee Mungu wangu; kwa sababu mji wako na watu wako wanaitwa kwa jina lako.*"

Kuwa na "*mfadhili*" inamanisha kuwa na huruma, hasa ule isiyo igwa.

Usambamba wa swala hili unapendekeza upendeleo huu unamanisha Baraka na kuwekwa na Bwana mara zote.

Labda inasisitiza kwamba Baraka kama hizi haziigwi, hata ivyo ni za lazima. Kama jinsi ambavyo dhabibu ya Bwana kwetu haikuigwa nab ado ilikuwa ni ya lazima.

"*BWANA akuinulie uso wake na kukupa amani.*" (Hes. 6:26).

"*Kuinua uso wake*" inaweza ikafanana na tabasamu.

Hivyo hupendekeza raha na kuridhika. Pia inathibitisha uhakikisho na utambulisho.

Neno "*amani*" haimanishi tu kukosekana kwa vita, bali hali ya kawaida ya kuwa salama au au faraja pamoja na uhusiano wetu na Mungu.

Kwa taifa la Israeli, Mungu aliwahidi amani kama wangekuwa waaminifu.

Law. 26:6, "*Nami nitawapa amani katika nchi, tena mtalala wala hapana atakayewatia hofu; name nitawakomesha wanyama wabaya katika nchi yenu, wala hautapita upanga katika nchi yenu.*"

Pia kulikuwa na amani kwa kila mmoja ambaye alimwamini Mungu.

Isa. 26:3, "*Utamlinda yeye ambaye moyo wake umekutegemea katika amani kamilifu kwa kuwa anakutumaini.*"

Kwamba Mungu angemruhusu Aruni na wanawe wawabariki wana wa Israeli kwa mausia yake yanayoonyesha kwamba Mungu hakika alitaka kuwabariki na kuwapa mahitaji yao.

Vipi kuhusu leo hii? Je Mungu anapenda kutubariki, na ikiwa ndiyo, kivipi?

Baraka ya kikuhani leo

"*BWANA akubarikie na kukulinda.*" (Hes. 6:24).

Hakika Bwana anatamani kutubariki!

Leo, Baraka hizo huja kupitia Yesu Kristo.

Efe. 1:3, "*Atukuzwe Mungu Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki kwa Baraka zote za rohoni, katika ulimwengu war oho ndani yake Kristo.*"

Zinakuja hasa kwa wale wanaoelezewa ndani:

Mat. 5:3-12, "*Heri walio maskini war oho maana ufalme wa mbinguni ni wao. Heri wenye huzuni maana hao watafarijika. Heri wenye upole maana hao watairithi inchi. Heri wenye njaa na kiu ya haki; maana hao watashibishwa. Heri wenye rehema maana hao watapata rehema. Heri wenye moyo safi maana hao watamwona Mungu. Heri wapatanishi maana hao wataitwa wana wa Mungu. Heri wenye kuudhiwa kwa ajili ya haki maana ufalme wa mbinguni ni wao. Heri ninyi watakapowashutumu na kuwaudhi na kuwanenea kila neno baya kwa uongo, kwa ajili yangu. Furahini na kushangilia kwa kuwa thawabu yenu ni kubwa mbinguni; kwa maana ndivyo walivyowaudhi manabii waliokuwa kabla yenu.*"

Na Bwana anatamani kutupatia mahitaji na kutujali, kama ilivyoelezwa na Yesu katika:

Mat. 6:25-32, "*Kwa sababu hiyo nawaambieni, msisumbukie maisha yenu, mle nini au mnywe nini, wala miili yenu mvae nini. Maisha je si zaidi ya chakula, na mwili zaidi ya mavazi? Waangalieni ndege wa angani ya kwamba hawapandi, wala hawavuni, wala hawakusanyi ghalani; na Baba yenu wa mbinguni huwalisha hao. Ninyi je! Si bora kupita hao? Ni yupi kati yenu ambaye akijisumbua aweza kujiongeza kimo chake hata mkono mmoja? Na mavazi ya nini kuyasumbukia? Fikirini maua ya mashamba jinsi yameavyo; hayafanyi kazi wala hayasokoti name nawaambia hata Sulemani katika fahari yake yote hakuvikwa vizuri kama moja wapo la hayo. Basi ikiwa Mungu huyavika hivi majani ya kondeni yaliyoko leo na kesho hutupwa kalibuni, je hatazidi sana kuwavika ninyi enyi wa imani haba? Msisumbuke basi mkisema tule nini? Au tunywe nini? Au tuvae nini? Kwa maana hayo yote mataifa huyatafuta; kwa sababu Baba yenu wa mbinguni anajua ya kuwa mnahitaji hayo yote.*"

Lakini kujali huku ni kwa masharti, sharti linaelezwa katika:

Mat. 6:33, "*Bali utafuteni kwanza ufalme wake , na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa.*"

Tafuta kwanza ufalme wa Mungu na haki yake, na baraka ya kikuhani itakuwa juu yako!

"*BWANA akuangazie nuru za uso wake, na kukuhifadhi.*" (Hes. 6:25)

Kama jinsi Baraka zote za kiroho huja kupiti Yesu, sasa neema ya Mungu inaonyeshwa kupitia Mwanaye.

Yoh. 1:17, "*Kwa kuwa torati ilitolewa kwa mkono wa Musa; neema na kweli zilikuja kwa mkono wa Yesu Kristo.*"

Ndiyo, Mungu anapenda kuonyesha tabasamu lake la huruma kwetu, lakini inamasharti ili kwamba tusiipokee bure.

2 Kor. 6:1-3, "*Nasi tukitenda kazi pamoja naye twawasihi msiipokee neema ya Mungu bure. Kwa maana asema wakati uliokubalika nalikusikia, siku ya wokovu nalikusaidia; tazama wakati uliokubalika ndiyo sasa; tazama siku ya wokovu ndiyo sasa. Tusiwe kwazo la namna yo yote katika jambo lo lote, ili utumishi wetu usilaumiwe.*"

Ni huzuni iliyoje kwamba neema ya Mungu hutolewa bure, alafu bado ni wachache wanaoukubali neema kama alivyokusudia!

"*BWANA akuinulie uso wake, na kukupa amani.*" (Hes. 6:26).

Kupitia Kristo, amani kwa Mungu sasa inawezekana.

Rum. 5:1, "*Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani, na mwe na imani kwa Mungu kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo.*"

Na tunapoendelea kuomba, Mungu anarejesha amani kupitia Mwanae.

Fil. 4:6-7, "*Msijisumbue kwa neno lo lote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu. Na amani ya Mungu wetu ipitayo akili zote, itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu.*"

Baba anatamani kutupa amani, lakini je tunaikubali?

Hitimisho

Tumekuwa tukizungumzia "Baraka ya Kikuhani" , jinsi Mungu alivyotaka kubariki Israeli chini ya Agano la Kale ukuhani wake katika ukuhani wa Aruni.

Tumegundua kwamba Baraka kama hizo zinapatikana pia leo; lakini Baraka za Mungu hutolewa kupitia Mwana wake, Yesu Kristo.

Ni nani leo aliye, "Kuhani wetu Mkuu".

Ebr. 4:14-16, "*Ili tusiwe tena watoto wachanga tukitupwa huku na kuchukuliwa na kila upepo wa elimu, kwa hila ya watu, kwa ujanja, tukizifuata njia za udanganyifu. Lakini tuishike kweli katika upendo na kukua hata tumfikie yeye katika yote, yeye aliye kichwa Kristo. Katika yeye mwili wote ukiungamanishwa na kushikanishwa kwa msaada wa kila kiungo, kwa kadiri ya utendaji wa kila sehemu moja moja, huukuza mwili upate kujijenga wenyewe katika upendo.*"

Kiwango cha somo hili ni rahisi, lakini bado ngumu:

Kama unatamani “Baraka ya Kikuhani” leo, lazima uwe katika Kristo na lazima naye awe Kuhani wako Mkuu; kwa maana hivyo ndivyo Mungu huwabariki watu wake leo!

Efe. 1:3, “*Atukuzwe Mungu Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki kwa baraka zote za rohoni, katika ulimwengu war oho ndani yake Kristo.*”

Je! Uko ndani ya Yesu Kristo? Mtu anaingiaje “ndani” ya Kristo, ambapo atapata baraka anazotoa kama Kuhani wetu Mkuu?

Zifuatazo ni hatua muhimu kufanya hilo liwezekane:

- **Imani.** Ebr.11:6,“*Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao.*” Nilipokuwa katika shule ya sekondari (nikiwa na miaka 17), kijana mmoja jirani yangu mwaka sawa na wa kwangu akaniambia kwamba alikuwa hamwamini Mungu, kwa vile nilikuwa nimebatizwa nilichukua nafasi kuongea naye kuhusu maandiko. Akaniambia kwamba anaona kuwa kuishi maisha ya Ukrsto ni nzuri, lakini hakuwa na uhakika kama Mungu yupo. Lakini ili awe sehemu salama labda anapaswa kwenda kanisani, na siku akifa na kusimama mbele za Mungu (kama kuna Mungu) siku ya hukumu (kama kuna hukumu), labda kama Mungu akiona kwamba alihudhuria kanisani na kuishi maisha mema kwamba Mungu atamruhusu kuingia mbinguni (kama kuna mbingu), na sio motoni (kama kuna moto). Nikamwambia “hayaendi hivyo. Unapaswa umwamini kwa moyo wako wote la sivyo huwezi kumpendeza.”

- **Toba**. Mdo. 2:38, “*Petro akawaambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*” Mdo. 11:18, “*…Basi Mungu amewajalia hata mataifa nao <u>toba liletalo uzima</u>.*” Kama ulikuwa unalala, ukasikia kelele kwenye chumba nyingine, na unafikiria mwenyewe, “kuna mwizi ndani ya nyumba hii!” hivyo unachukua simu ya mkononi, taratibu unawapigia polisi, ukiwaambia kwamba kuna mwizi ndani kwako, na unawapa anwani yako. Muda kidogo unawasikia polisi wamefika na kumkamata mwizi. Anapiga kelele, “Samahani, Samahani!” anaomba msamaha wa nini? Anaomba msamaha kwa sababu amekamatwa; na sio kwamba ameiba. Katika toba ya kweli mwizi angeomba msamaha kwamba hataibatena na kwamba anataka kubadili maisha yake ili kwamba asiibe tena. Hiyo ndio toba ya

kweli. Ni badiliko la nia linaloongoza katika badiliko la tendo. tunapaswa kufanya hivyo kabla hatujafanyika Wakristo.

- **Kiri.** Rum. 10:9-10, "*Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu utaokoka. Maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu.*" Tunakiri nini? Kwamba tunaamini kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu.

  Kumbuka andiko hilo hapo juu kwamba (kuamini), toba, na kukiri ni "**KATIKA**" haki, uzima au wokovu. "Katika" inamanisha kuelekea katika kutu fulani; sio kwamba mtu tayari ameshapata.

- **Ubatizo.** Ni katika ubatizo ambapo haki, uzima, na wokovu hupatikana. Yesu mwenyewe alibatizwa kuitimiza haki yote, "*Lakini Yohana alitaka kumzuia akisema, mimi nahitaji kubatizwa na wewe nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia, kubali hivi sasa kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akamkubali. Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini; na tazama mbingu zikamfunukia akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu yake; na tazama sauti kutoka mbinguni ikasema, huyu ni mwanangu mpendwa wangu, ninaye pendezwa naye.*" (Mat. 3:14-17). Yesu alibatizwa kwa sababu Mungu alisema kwamba ni kitu sahihi kufanya. Unaona jinsi Mungu alivyopendezwa wakati Yesu alipobatizwa? Yesu pia akasema, "*Ndivyo **itupasavyo** kuitimiza haki yote.*" Tunabatizwa kwa sababu inatiza haki yake, na sio kwa sababu ya haki yetu.

  Hakika, tusipobatizwa, bado tungali katika dhambi zetu. "*Petro akawaambia tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*" (Mdo. 2:38). Petro, umesema kusudi la ubatizo ni nini? "*kwa ajili ya ondoleo la dhambi zenu".* Kwa nini mtu aache atua hii muhimu inayoondoa dhambi zetu?

  Yesu aliagiza kwamba ili kuufikia wokovu lazima tubatizwe. "*Akawaambia enendeni ulimwenguni mwote mkahubiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye **na** kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa.*"

  Anania alimwambia Sauli (kabla hajaitwa Paulo) kitu kama hiki, "*Basi sasa unakawilia nini? Simama ubatizwe ukaoshwe dhambi zako, ukiliitia jina lake.*" (Mdo. 22:16). Ubatizo ni hitaji ambalo Mungu ametupatia.

Ubatizo unaitwa maziko. "*Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima.*" (Rum. 6:4). Utu wetu wa kale lazima ufe. "*Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, viyvo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama tulivyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika tutaunganika kwa mfano wa kufufuka kwake; tukijua neno hili ya kuwa utu wetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike tusitumikie dhambi tena;*" (Rum. 6:3-6). Ubatizo ni ramani ya Mungu inayotumika katika damu ya Kristo katika maisha yetu kwa ubatizo. Tuko huru na dhambi zetu za kale pale tu tunapo batizwa.

Hii haimanishi "kunyunyiza. Andiko hilo hapo juu linasema ubatizo ni maziko. Hatupeleki mwili makaburini na kuuwekea udongo kidogo juu yake; bali tunauzika.

Kama haujafanyika Mkristo, kwa nini usifanyike leo.